HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA

# TOLEO MAALUM MWENGE WA UHURU-2024

## TAASISI ZA UMMA ZAAGIZWA KUTUMIA MFUMO WA NeST KWA MANUNUZI



## JIWE LA MSINGI LAWEKA OFISI YA MANISPAA YA SINGIDA






## KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE ATOA ZAWADI KWA WANANCHI WA MANISPAA SINGIDA

## KUELEKEA UCHAGUZI WANANCHI WAASWA KUKATAA VIONGOZI WATOA RUSHWA



## KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU: 'KATAENI VIONGOZI WATOA RUSHWA'

Wananchi wa Manispaa ya Singida, wameaswa kutothubutu kuchagua wagombea ambao watatoa rushwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwani kwa kufanya hivyo kutasababisha uwepo wa viongozi wabovu watakaochelewesha maendeleo yao wenyewe. Kauli hiyo imetolewa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge Uhuru kitaifa, Godfrey Eliakimu Mnzava baada ya kupokea Risala ya Utii kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan, katika uwanja wa Bombadia, Manispaa ya Singida. Amesema viongozi bora ni wale wenye sera na mipango madhubuti na sio viongozi wapenda rushwa ambao wanatanguliza maslahi binafsi badala ya wananchi wao. "Msichague viongozi wanaotoa rushwa watawarudisha nyuma kwa sababu hawataleta maendeleo bali watajiangalia wao tu." Tanzania inatarajia kufanya uchaguzi wa viongozi Serikali za Mitaa, Novemba mwaka huu.

# DC GONDWE APOKEA MWENGE WA UHURU MANISPAA YA SINGIDA



.Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhe Godwin Gondwe amepokea rasmi Mwenge wa Uhuru kwa 2024 katika Manispaa ya Singida baada ya kukabidhiwa na Mkuu Wilaya ya Ikungi, Mhe. Thomas Apson.

Makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru kwa wilaya hizo mbili yalifanyika Julai 8, 2024 katika eneo la Kisaki, saa 2 asubuhi.

Mwenge huo wa Uhuru utakimbizwa kwa umbali wa kilomita 88, utatembelea miradi saba maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 74.6. pamoja na kupokea taarifa tano za utekelezaji wa program.

Miradi itakayotembele ni ujenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, ujenzi wa Ofisi za Manispaa ya Singida, Ufunguzi wa Barabara ya Minga, Kituo cha Afya Mtipa, mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kutibu Majitaka, Kiwanda cha Mafuta Alizeti, Kikundi cha Vijana cha ANACO GYPSUM na Chuo cha watu wenye Ulemavu.



*Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Godfrey Eliakimu Mnzava akizindua Klabu ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa alipotembelea Chuo cha Watu Wenye Ulemavu.*

## TAASISI ZA UMMA ZAAGIZWA KUTUMIA MFUMO WA NeST KWA MANUNUZI

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024, Godfrey Eliakimu Mnzava, amezitaka taasisi za umma kuzingatia matumizi ya Mfumo wa Ununuzi wa Umma (NeST) wakati wa kufanya manunuzi ili kuweka uwazi na uwajibikaji.

Kiongozi huyo amesema hayo wakati akizungumza na wananchi wa Manispaa ya Singida (Julai 8, 2024) baada ya Mwenge wa Uhuru kukagua barabara ya Minga yenye urefu wa kilometa 1.21 iliyojengwa kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Sh. 992,096,092.

Mnzava amesema Rais Samia Suluhu Hassan ameendelea kuelekeza manunuzi ya umma kufanyika kupitia mfumo wa NeST ambao unasimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) lengo likiwa ni kuweka uwazi, uwajibikaji na kudhibiti manunuzi ya umma.

Amesema kupitia mfumo huo wazabuni mbalimbali wanaomba zabuni moja kwa moja, washindi wa zabuni kujulikana kupitia mfumo.

"Kumekuwa na malalamiko kwamba kuna watu wanapendelewa kupewa zabuni lakini kupitia mfumo wa NeST hakuna cha upendeleo kwani unaona kitu gani umekidhi na kipi haujakidhi," amesema Mnzava.

Aidha,Mnzava amepongeza Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) Manispaa ya Singida kwa kuzingatia manunuzi kupitia mfumo wa NeST ambayo ni maelekezo ya serikali katika suala la manunuzi.

Awali Meneja wa TARURA Manispaa ya Singida, Mhandisi Lazaro Kitomari amesema mradi wa barabara ya Minga kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 1.21 umejengwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ikiwa ni sehemu ya fedha inayotolewa kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya barabara.



Amesema TARURA imetekeleza mradi huu wa barabara kwa kiwango cha lami katika awamu tatu,awamu ya kwanza ilijenga kilometa 0.6 katika mwaka wa fedha 2021-2022, awamu ya pili i kilometa 0.61 mwaka wa fedha 2022-2023 na awamu ya tatu mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo TARURA imefunga taa za barabarani 37 mradi huu kwa awamu zote umegharimu jumla ya sh.mil 992,096,092.

## MWENGE WA UHURU WAWEKA JIWE LA MSINGI CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA

Mwenge wa Uhuru umeweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Kampasi ya Singida, Halmashauri Manispaa ya Singida Jiwe hilo limewekwa na kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Godfrey

Eliakimu Mnzava baada ya kukagua na kupitia nyaraka muhimu za jengo hilo ambao ujenzi wake unaendelea.
Mnzava alisema:"Tumepitia na kukagua utekelezaji wa mradi pamoja na nyaraka mbalimbali na masuala yote muhimu kuhusiana miradi kama ambavyo serikali inaelekeza... mfanyie kazi yale ambayo tumeelekeza."
Mradi wa ujenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma unatekelezwa kwa gharama ya sh bilioni 1.3 fedha ambazo zimetengwa katika bajeti ya 2022-23 na 2023-24.



## ‘UJENZI WA OFISI ZA MANISPAA UKAMILIKE KWA WAKATI'




Halmashauri ya Manispaa ya Singida imetakiwa kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi za Halmashauri hiyo kwa wakati, ilikuendelea kutoa huduma kwa wananchi. Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Godfrey Eliakimu Mnzava alisema hayo wakati akiweka jiwe la msingi katika mradio huo, baada ya kukagua na kutembelea kuona maendeleo ya ujenzi na kupitia nyaraka mbalimbali.

"Ujenzi ukamilike kwa wakati na lengo la serikali ya awamu ya sita ni kuona inakuwa na miundombinu bora kwa kuhakikisha kuna na majengo yenye hadhi ya awamu ya sita na watumishi wanafanya kazi katika mazingira mazuri na wananchi wanapata huduma bora."

Kwa upande wa Mkuu wa Divisheni ya Utumishi na Utawala, Manispaa ya Singida, Edward Mboya, katika taarifa yake amesema Halmashauri ya Manispaa ya Singida ilipokea Sh. Bilioni 2 kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi mpya za Manispaa kutokana na uchakavu wa jengo lilnalotumika kwa sasa na kushindwa kukidhi mahitaji yaliyopo. Amesema katika mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Manispaa ilipokea Kiasi cha Sh. Bilioni moja kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa awamu ya kwanza na mwaka wa fedha wa 2023/2024 zilipokelewa Sh.bilioni moja utekelezaji wa ujenzi wa awamu ya pili.



## MRADI WA UHIFADHI WA MAZINGIRA WAPONGEZWA-MANISPAA YA SINGIDA

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru wa Kitaifa, Ndugu Godfrey Eliakimu Mnzava amepongeza utekelezaji wa mradi wa Uhifadhi wa Mazingira na kutoa maelekezo juu ya upandaji miti.

pongezi hizo zimetolewa Julai 8, 2024 wakati akiweka jiwe la msingi katika mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya kutibu Majitaka na kupokea taarifa ya upandaji miti.

Mnzava ameelekeza kuwa wanafunzi wanapoanza darasa la kwanza na kidato cha kwanza kuhakikisha wanapanda miti na kuitunza mpaka pale wanamaliza masomo, aidha ameagiza vibali vya ujenzi utoaji wa vibali vya ujenzi uende sambamba na usimamizi wa upandaji miti katika eneo la mteja.

"Hongereni kwa kazi nzuri katika upandaji wa miti kikubwa tuendelee kusimamia na kutunza miti ambayo imepandwa kwa ni sehemu ya utunzaji wa mazingira kama ambavyo kauli mbiu inavyosisitiza."

Katika taarifa za Uhifadhi wa Mazingira ambayo iliwasilishwa na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira, Jacob Chibuga kwa mwaka 2023-24 jumla ya miti 1,345,000 imepandwa ikiwa ni sawa na asilimia 89.7 ya lengo ambalo ni kupanda miti 1,500,000 ndani ya Manispaa ya Singida.






## "VIJANA WAJULISHWE YANAYOTEKELEZWA NA SERIKALI"

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Ndugu Godfrey Eliakimu Mnzava amepongeza Kongamano la Vijana ambalo amelitaja kuwa bora kati ya halmashauri 99 alizopita na kusisitiza vijana kufahamishwa mambo yanatokelezwa na Serikali ya awamu ya sita.

Hayo yamesemwa leo Julai 8, 2024 katika Kongamano la Vijana ambalo limefanyika katika Uwanja wa Bombadia, Manispaa ya Singida ambapo Mkesha wa Mwenge wa Uhuru ulifanyika na maada mbalimbali zilitolewa na wataalum waliobobea akiwemo Mwenyekiti wa UVCCM, Taifa, Comrade Mohamed Kawaida.

Baadhi ya maada ambazo zilitolewa katika Kongamano hilo ni pamoja na Elimu ya Mpiga Kura, Falfasa ya Mwenge wa Uhuru, Elimu ya Utunzaji fedha, Wajibu wa Kijana.

Vijana zaidi ya 1000 kutoka kata 18 za Manispaa ya Singida walishiriki katika Kiongozi wa Mwenge wa Uhuru Kitaifa amekiri kufurahishwa na namna kongamano la vijana lilivyofana na ushiriki mkubwa wa viongozi na wadau mbalimbali.

"... niwapongeze sana kwa Kongamano hili katika Halmashuri 99 nilizopita hapa naona mmefanya vizuri kuwa na vijana zaidi ya 1000 ninaamini watakuwa wamejifunza kitu." amesema.

Mnzava amesema makongamano kama haya ni muhimu kwa vijana, kwani yanawapa nafasi ya kujifunza mambo mengi ya msingi kwa maendeleo ya taifa letu.

Aidha amesisitiza uendelevu wa makongamano ya vijana ilikuwajengea uwezo na kuwaimarisha uzalendo.





# ‘PICHA ZA MATUKO MBALIMBALI YA MWENGE WA UHURU MANISPAA YA SINGIDA













# ‘PICHA ZA MATUKO MBALIMBALI YA MWENGE WA UHURU MANISPAA YA SINGIDA










